



**SWAHILI B – HIGHER LEVEL – PAPER 2**  
**SWAHILI B – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 2**  
**SWAHILI B – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 2**

Thursday 3 November 2005 (morning)

Jeudi 3 novembre 2005 (matin)

Jueves 3 de noviembre de 2005 (mañana)

1 h 30 m

---

**INSTRUCTIONS TO CANDIDATES**

- Do not turn over this examination paper until instructed to do so.
- Choose one task.

**INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS**

- Ne retournez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Choisissez une tâche.

**INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS**

- No dé la vuelta al examen hasta que se lo autoricen.
- Elija una tarea.

*Andika maneno yasiyopungua 400 juu ya mojawapo ya haya yafuatayo.*

1. Fasihi ni kioo ya jamii. Kupitia kwayo mwandishi huangaza matatizo mbalimbali ya kijamii. Andika insha ukijadili kauli hii kwa kutumia mifano mbalimbali ya mojawapo wa kazi za fasihi ulizowahi kuzisoma.
2. Shule yako imeamua kuifadhili shule nyingine iliyo kwenye maeneo maskini kwa kukusanya pesa na kutoa huduma za bure. Ili kuuzindua mpango huu, umealikwa kutoa hotuba juu ya mada ifuatayo ‘Elimu ni ufunguo wa maisha’ mbele ya walimu na wanafunzi wa shule zote mbili. Andika hotuba yako.
3. Kwenye miaka ya hivi karibuni, viwango vya elimu shulenii mwako vimeshuka mno. Mwalimu mkuu ametatizwa mno na hali hii na amewauliza wanafunzi kuandika ripoti fupi kuelezea sababu za shida hii. Andika ripoti yako.
4. Gazeti la kitaifa linapanga mashindano ya kueneza habari juu ya majukumu mbalimbali ya kijinsia katika jamii za Kiafrika. Washirika wameulizwa kuandika mapendekezo yao juu ya njia mbalimbali ambazo zinaweza kutumiwa kuleta usawa kati ya wanaume na wanawake barani Afrika. Pendekezo bora litachapishwa kwenye gazeti. Andika pendekezo lako.
5. Shule yako imechaguliwa kuandaa mashindano ya nyimbo, na michezo ya kuigiza ya mwaka huu. Wewe ukiwa mwanachama wa kamati inayoshughulikia maandalizi ya sherehe hizi umeombwa kuandika tangazo litakolotolewa kwenye mojawapo wa magazeti nchini mwako ukiwalika watu kuhudhuria mashindano haya. Andika tangazo lako.
6. Endeleva hadithi ifuatayo: Nilikuwa nimejibwaga kwenye kitanda ili angalau nipate lepe la usingizi kama yalivyokuwa mazoea yangu kila Jumamosi alasiri. Lakini baada ya kitambo kifupi nilizunduliwa na kelele nyingi.